HOTUBA YA AFISA MTENDAJI MKUU WA JATU PLC, NDUGU PETER ISARE KATIKA HAFLA YA KUORODHESHWA KWA HISA ZA JATU PLC KWENYE SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM, TAREHE 23 NOVEMBA, 2020

Ndugu Mgeni Rasmi, CPA. Nicodemus Mkama, Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA);

Ndugu Moremi Marwa, Afisa Mtendaji Mkuu wa Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE);

Ndugu Benitho Kyando, Afisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Uhifadhi wa Dhamana (CSDR);

Ndugu Eliakimu Mtawa, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Vijana Ofisi ya Waziri Mkuu;

Ndugu Revelian Ngaiza, Mratibu wa Mkakati wa kilimo wa Vijana Kitaifa;

Ndugu Eng. Dkt. Zaipuna Yonah, Mwenyekiti wa Bodi ya JATU Plc;

Afisa Watendaji na Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi Mliohudhuria hapa;

Menejimenti na Wafanyakazi wa JATU PLC;

Wawakilishi wa Vyombo vya Habari;

Wageni Waalikwa;

Mabibi na Mabwana;

Ndugu Mgeni Rasmi, Napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kuwa mgeni rasmi na kuweza kujumuika nasi katika hafla hii ambayo ni ya kihistoria katika safari ya JATU Plc. Aidha, ninawashukuru wadau wote kwa kuweza kutenga muda na hatimaye kushiriki katika hafla hii ili kushuhudia tukio la kihistoria katika ukumbi huu wa Soko la Hisa Dar es salaam(DSE), ambapo leo tutashuhudia hisa za kampuni ya kwanza Tanzania iliyoanzishwa na vijana wazalendo wa kitanzania ambao hawajawahi kuajiriwa katika mfumo rasimi wa ajira, zikiorodheshwa katika soko la hisa. Ajenda kuu ya Kampuni yetu ni kilimo biashara na kukuza viwanda vinavyotumia malighafi zinazozalishwa kutoka katika mashamba yanayomilikiwa na kuendelezwa na kampuni yetu, kwa lengo la kutengeneza ajira kwa watanzania na hatimaye kuchangia katika kukuza uchumi wa nchi yetu. JATU ni kufupi cha Jenga Afya Tokomeza Umasikini na Dhima ya Kampuni yetu ni kujenga afya na kutokomeza umaskini kwa kutumia rasilimali watu, kilimo na Viwanda. Wadau mliohudhuria katika hafla hii tunaamini wengi wenu ni mashuhuda na mabalozi wa JATU Plc kwa kuwa mmekuwa wateja wetu na sehemu ya historia ya mafanikio ambayo yamekwisha patikana mpaka sasa.

Ndugu Mgeni Rasmi, JATU Plc ni matokeo ya elimu tuliyoipata katika chuo kikuu cha Dar es salaam ambapo tulifundishwa namna ya kushiriki katika miradi ya kijamii na kutengeneza mtaji kupitia soko la mitaji. Tukiwa wanafunzi hapo chuoni Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (Capital Markets and Securities Authority - CMSA), chini ya uongozi wa CPA. Nicodemus Mkama walianzisha shindano maalumu ambalo lililenga kuwafundisha na kuwajengea uwezo wanafunzi wa vyuo vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu lililojulikana kama Capital Markets Universities and Higher Learning Institutions Challenge, namna ya kuwekeza katika masoko ya mitaji na kuibua miradi katika nyanja za kilimo, viwanda na teknolojia ya habari na mawasiliano. Tukiwa kama vijana ambao tulipata uelewa wa namna bora ya kupata mtaji kupitia masoko ya mitaji, mimi Peter Isare (MD), Mohamed Simbano (GM) pamoja na wenzetu tuliona si vyema kuishia kwenye nadharia ya shindano, na hivyo tukaamua kuanzisha kampuni ambayo tuliamini siku moja itauza hisa kwa umma na kuorodheshwa katika soko la hisa la Dar es salaam kwa lengo la kuwanufaisha watanzania wote hivyo kufanya mambo kwa uhalisia. Kwa njia ya kipekee na moyo wa dhati, leo nipo mbele yenu wadau wa masoko ya mitaji na watanzania wote kwa ujumla kuwashuhudia kwamba kampuni hiyo iliyokuwa kwenye nadharia, ilianzishwa na leo inaorodheshwa rasmi katika soko la hisa la Dar es

saalam ikiwa na jina la JATU PLC na tumekidhi matakwa ya sheria na kanuni za masoko ya mitaji (CMSA) na Sheria na Kanuni za Soko la Hisa (DSE). Hakika historia leo inaandikwa, wote mliowezesha mtabaki katika mioyo yetu, na mioyo ya watanzania wote, hususani vijana. Mwenyezi mungu awabariki wote. Mungu ibariki serikali na viongozi wanaoguswa na maendeleo ya maisha ya watanzani kiuchumi, chini ya uongozi bora wa Rais wetu Mh. Dkt John Pombe Magufuli.

Ndugu Mgeni Rasmi, JATU Plc ni kampuni ya kitanzania ambayo inamilikiwa na vijana, akina mama na watu wa kipato cha kawaida. Kupitia JATU Plc maelefu ya watanzania wameweza kushiriki katika miradi mikubwa ya pamoja katika kilimo, viwanda, masoko na Tehama. Kampuni hii imefanikiwa kuanzisha mashamba makubwa yenye jumla ya hekari 17,678 katika mazao muhimu ya chakula kama vile mahindi, mpunga, alizeti, maharage, machungwa, parachichi na aina nyingi za mboga mboga na matunda katika mikoa mbali mbali Tanzania ambayo ni Manyara, Morogoro, Tanga, Ruvuma, Singida na Njombe. Takribani tani 8,670 za nafaka huchakatwa katika viwanda vya JATU Plc vilivyopo Mbingu Morogoro na Kibaigwa Dodoma, hatimaye kuuzwa kupitia maduka makubwa yanayomilikiwa na JATU Plc yaani JATU

Supermarkets zilizopo mikoa ya Arusha, Mtwara, Mwanza, Dar es salaam na Dodoma.

Ndugu Mgeni Rasmi, JATU Plc ni kampuni ya vijana wazalendo wa kitanzania ambao hawakuwahi kuajiriwa kabla. Kwa kutambua na kuzingatia umuhimu wa vijana wenzetu, tumefanikiwa kutengeneza ajira takribani 10,650 ambazo zinajumuisha ajira za kudumu, ajira za muda mfupi na ajira zitokanazo na majukumu ya kila siku katika miradi na ofisi za kampuni zilizopo katika mikoa 12 Tanzania. Tumetambua umuhumi wa kina mama na wanawake katika maendeleo ya kampuni na ndiyo maana zaidi ya asilimia 46 ya wafanyakazi wa kudumu wa JATU Plc ni vijana wa kike na tunashukuru Mungu wanafanya kazi kwa bidi na uaminifu mkubwa hadi kampuni yetu leo imefikia hatua hii kubwa.

Vilevile, JATU Plc kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano imewekeza vyema na kutengeneza mifumo ambayo imerahisisha huduma na kuwezesha watumiaji zaidi ya 76,999 kunufaika na bidhaa za JATU plc na kutengeneza kipato cha kila siku kutokana na mfumo wetu wa masoko ambao unamtengenezea mteja faida kutokana na manunuzi yake, na kwa kuwa tunahusika na bidhaa za chakula cha kila siku, kwetu hii inaitwa KULA ULIPWE. Kula ulipwe inawezekana tu

kama utanunua bidhaa zilizozalishwa na kampuni ya JATU plc na ukazinunua kupitia mfumo wetu rasmi wa kielectronic ambao ni app ya JATU Market. Pia tunazo app zingine kama vile “JATU Pesa” na “JATU Talk” ambazo zinamwezesha kijana mbunifu mwenye wazo kupata mtaji kwa kushirikiana na JATU ndoto yake inatimia.

Ndugu Mgeni Rasmi, baada ya kueleza mambo yaliyofanyika mpaka sasa, napenda kuweka bayana kwamba, kufuatia JATU Plc kuorodheshwa katika soko la hisa, tunatarajia kutekeleza mpango biashara ambao unahusisha miradi mikubwa zaidi kwa kushirikiana na jamii, ambapo tunatarajia kubadilisha maisha ya maelfu ya watanzania, hususani vijana na akina mama. Tunategemea kuongeza ubunifu zaidi katika kilimo na miradi ambayo itapelekea kuwa na viwanda vingi vya kuzalisha bidhaa ambazo tutaziuza kupitia mifumo yetu. Tutaboresha miundombinu katika miradi yetu ya kilimo na tutahakikisha tunafanya kilimo cha kisasa kwa kutumia wataalamu na zana za kisasa ili kuongeza mavuno. Tutajenga viwanda vya kisasa ambavyo vitakuwa na teknolojia bora katika maeneo ya miradi yetu na hasa vijijini ili kuwagusa hata wale vijana walioko vijijini. Tutawekeza zaidi katika Tehama maana tunaamini katika dunia ya sasa Tehama ina uwezo wa

kubadilisha maisha ya watu wengi na hivyo kujenga ajira nyingi zaidi za kudumu katika nchi yetu.

Ndugu Mgeni Rasmi, vilevile tumeanzisha program inaitwa JATU Talk, ambapo tunamkutanisha kijana mwenye wazo la kilimo biashara na mtaji. Baada ya kuorodheswa katika soko la hisa tunategemea kuweka nguvu kubwa hapa ili kuwafikia vijana wabunifu wengi zaidi na hatimaye kuwa na kampuni kubwa ya umma yenye wawekezaji wengi, hivyo kuongeza ukwasi kwenye soko la hisa. Tunatamani kila kijana aweze kuwekeza na kumiliki hisa za JATU Plc, ili kupata manufaa yatokanayo na kampuni yetu.

Ndugu Mgeni Rasmi, ninapoelekea mwishoni, napenda kutoa wito kwa watanzania, wazee, akina mama, akina baba, vijana pamoja na wote ambao wanapenda kuwekeza na kukuza uchumi, JATU Plc imekuja kwa ajili yenu, sasa ni muda muafaka wa kutumia fursa zilizopo katika masoko ya mitaji na kuunganisha nguvu kupitia JATU Plc ili tuweze kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja na hatimaye uchumi wa taifa kama mheshimiwa rais anavyotuasa. Tuzitambue rasilimali tulizonazo ili tuzitumie vyema hakika tutaweza kuutawala uchumi wetu sisi kama wazawa.

Lakini pia nitumie fursa hii kuwakumbusha wale watanzania ambao wako nje ya nchi, sisi kama JATU Plc tumefanya utafiti na kugundua kwamba watanzania wengi walio nje ya Tanzania wanapenda kuwekeza nchini hasa katika kilimo lakini kwa muda mrefu walikosa mfumo (platform) mzuri wa kushiriki moja kwa moja, sasa tunawahakikishia, JATU Plc imekuja kutatua tatizo hilo, na sasa mnaweza kushiriki katika miradi ya kilimo na viwanda. Tembelea na mjifunze mfumo wa JATU Plc mtagundua tumewaletea fursa muafaka na maridhawa, kwani ukiwa kama muwekezaji wa JATU huhitaji kusubria tu gawio la mwisho wa mwaka katika hisa ndo uone faida, unaweza kupata faida kwa kulima na JATU mazao ambayo yanazalishwa na viwanda vya jatu, lakini pia unaweza kuwa wakala msambazaji wa bidhaa za jatu au mtumiaji na kila mwezi utatengeneza kipato cha kukuza uchumi wako.

Ndugu Mgeni Rasmi, Uongozi wa JATU Plc unatambua kwamba baada ya kuorodheshwa katika soko la hisa, tunapaswa kuendelea kukidhi matakwa ya sheria na kanuni za soko la hisa (DSE) na Mamlaka ya Masoko ya mitaji na Dhamana (CMSA) ili kulinda na kusimamia maslahi ya wawekezaji. Sisi viongozi wa JATU Plc tunaahidi na tunakuhakikishia tutafanya kazi kwa uwazi, ubunifu, bidii na uaminifu ili

kutengeneza faida kubwa kwa kampuni na kuongeza thamani ya uwekezaji wa wanahisa.

Ndugu Mgeni Rasmi, kwa namna ya pekee na moyo wa dhati ninakushukuru sana CPA. Nicodemus Mkama na viongozi wengine wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kwa kutupa elimu, miongozo na kutulea hadi leo tumefanikiwa kufika hatua hii. Aidha, nashukuru uongozi wa Soko la Hisa la Dar es salaam chini ya uongozi wa Ndugu Moremi Marwa kwa juhudi zao za kila siku kuhakikisha tunatimiza vigezo vyote vya kuingia soko la hisa, nawashukuru Ofisi ya Waziri Mkuu kwa malezi yao ya muda mrefu na ya kudumu wanayo toa kwa JATU, niwashukuru na kuwapongeza Wizara ya Kilimo kwa mchango mkubwa wanaoipa JATU katika kutekeleza miradi ya kilimo maeneo mbalimbali ya Tanzania. Niwashukuru sana wajumbe wa bodi ya wakurugenzi wa kampuni ya JATU Plc, niwashukuru wanahisa wote pamoja na wafanyakazi wa JATU Plc kwa ubunifu wao muda wote ambao umekuwa chachu ya mafanikio ya kuwezesha kuorodheshwa kwa JATU Plc katika soko la Hisa. Vilevile, ninawashukuru Kampuni ya ARCHO Ltd, Kampuni yenye Leseni ya Ushauri wa Uwekezaji kutoka CMSA, ambao wamekuwa walezi waelekezi (Nominated Advisors - NOMAD) wa JATU Plc katika mchakato mzima wa kuorodhesha hisa,

chini ya uongozi wa Ndugu IYEN Nsemwa, Mkurugenzi Mtendaji wa Archo Ltd.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.